**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI CHIUNGUTWA MWAKA ……………

**Mkuu wa Shule:-0717396715/ 0789138283**

**Makamu Mkuu wa Shule:- 0682580219**

**Matron/Patron:- 0766375615**

**Shule ya Sekondari Chiungutwa**

**S.L.P. 64 - MASASI**

**Tarehe……………**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi …………**
**……………………………………………..**
**S.L.P …………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI CHIUNGUTWA HALMASHAURI YA WILAYA MASASI, MKOA MTWARA, MWAKA ………**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka na atasoma tahasusi ya ……………....................

Shule ya Sekondari CHIUNGUTWA ipo umbali wa Kilometa 30 Mashariki mwa Mji wa MASASI, Usafiri wa basi kutoka mjini MASASI unapatikana katika kituo cha mabasi KAUMU Nauli ni Shilingi 5000, kwa pikipiki ni Shilingi 10,000/=, kwa bajaji. 20,000/=

Muhula wa Masomo unaanza tarehe……………. hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe……….. Mwisho wa kuripoti ni tarehe……………. Pia kutakua na usafiri wa Pamoja wanaotoka DAR – ES – SALAAM na mikoani wakati wa kufika shuleni.

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

i. Sare ya shule hii ni suruali ndefu rangi ya kijivu nyeusi. Chini inchi saba na rinda mbili pindo nchi 18, kwa wasichana sketi za kijivu nyeusi (dark grey) mshoni rinda box kubwa katikati na mawili pembeni sketi ndefu iguse kifundo cha mguu.
ii. Mashati mawili rangi nyeupe mikono mirefu aina ya tomato kwa wasichana na wavulana kwa wanaovaa juba wanaweza kushona nusu kanzu
iii. Sare ya Michezo ni track suit rangi ni bluu bahari jozi moja
iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi na raba nyeupe kwa ajili ya michezo jozi moja;
v. Soksi jozi mbili nyeusi kwa wavulana na nyeupe kwa wasichana.
vi. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;
vii. Sweta rangi ya kijivu nyeusi (dark grey) moja

viii. Nguo za kushindia suruali nyeusi mbili (suruali zishonwe kama zile za darasani hapo juu) na tisheti ya zambarau yenye kola kwa ajili ya kushindia , kwa wasichana gauni ya zambarau la solo mikono mifupi ya shati kwa

ix. wale wanaovaa juba waje na juba la bluu (bluu shule) kwa ajili ya kushindia na juba jeupe kwa ajili ya darasani

x. Tisheti (T-shirt) mbili rangi ya bluu kwa ajili ya darasani zenye kola zinapatikana shuleni

**NB**: **VIFAA HIVYO VINAPATIKANA DUKA JIRANI NA SHULE**

xi. Aje na result slip na cheti cha kuzaliwa.

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari kumi na mbili counter book quire three
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka; (wanafunzi wote)
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (vilivyotungwa na TIE)
iv. Scientific Calculator;
v. Godoro Ft 6 kwa $2^1/_2$
vi. Mashuka Jozi 2 bluu kwa wavulana na shuka za pink kwa wasichana , foronya ya godoro 1, chandarua 1
vii. Nguo za ndani za kutosha;
viii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
**ix.** Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko**; (MICHEPUO YOTE)**
**x. Vifaa vya usafi (VINAPATIKANA DUKA JIRANI NA SHULE**
(a) Kwanja 1, (**michepuo yote)**
(b) Reki **(michepuo yote )**
(c) Jembe **(michepuo yote)**
(d) Mopa **(HGL & HGLi )**
(e) Fagio ngumu za kusugulia chooni **(HKL & HGFa)**
(f) Fagio za nje (Chelewa) (**MICHEPUO YOTE)**
(g) Sabuni ya maji lita tano (**MICHEPUO YOTE)**
xi. Tochi kwa ajili ya kutumia pale umeme unapokatika
xii. Aje na pasi ya mkaa kwa ajili ya kunyoshea nguo
xiii. Aje na kiti kimoja cha plastic rangi ya bluu (**MICHEPUO YOTE)**
xiv. Awe amekatiwa bima inayoweza kutumika hospitali yeyote zahanati hadi hospitali ya rufaa kama hana atakatiwa shuleni kwa gharama ya **Tshs 50,400/=** tu aje nayo cash.
xv. Aje na sabuni ya maji lita tano kwa ajili ya usafi
xvi. Mwanafunzi afunguliwe akaunti kwenye benki ya NMB kwa ajili ya kutumiwa na kuhifadhi fedha yake kwamwe hairuhusiwi fedha kutunzwa kwa mwalimu au mtumishi yeyote.

**2.3 Michango mbalimbali**

**a) Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

***Fedha ilipwe kwenye akaunti No 70501200105 jina la akaunti Chiungutwa Sekondari Kuungwa kwenye kundi la WATSSAP la wazazi wasiliana na namba 0715916958 na usafiri wa pamoja***

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na

xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kufuga ndevu;
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
viii. Uvutaji wa sigara;
ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
x. Kusababisha mimba;
xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xiv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvi. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**PRIME MINISTER'S OFFICE**

**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

**MASASI DISTRICT COUNCIL**

CHIUNGUTWA SECONDARY SCHOOL

P.O.BOX 64,

MASASI

DATE………………………………….

REF.NO……………

THE MEDICAL OFFICER

……………………………………

……………………………………

……………………………………

**PUPIL FORM FOR MEDICAL EXAMINATION**

Please examine the above named student to his fitness as indicated below. This certificate must be signed by qualified medical officer of a Government hospital or Health centre

1. stool…………………………………………………….
2. Urine ……………………………………………………..
3. general diseases…………………………………………
4. T.B…………………………………………………
5. Eye………………………..…………………………………..
6. Ear ………………………………………………………….
7. Chest ……………………………………………….
8. Abdomen ………………………………………………………………
9. Skin ………………………………………………………………..
10. Any other disability………………………………………………………….

I certify that above is fit/not fit to pursue secondary education as indicated above.

NAME OF MEDICAL OFFICER…………………………………………….

SIGNATURE OF MEDICAL OFFICER……………………………………………….

STATION………………………OFFICIAL STAMP

DATE……………………………………………………

**CHIUNGUTWA SEKONDARI S.1338**

**FOMU YA HISTORIA YA MWANAFUNZI**

1. (a) Jina la mwanafunzi………………………………………………………………..

   (b ) mchepuo wake………………………………………………………………..

2. Je mwanafunzi anamatatizo ya kiafya ya kudumu?

   A. NDIYO ☐ weka √ au *X* kwenye kisanduku

   Ainisha matatizo hayo ya kiafya

   (i) ………………………………………………………………………………

   (ii) ………………………………………………………………………………….

   (iii) ………………………………………………………………………………….

   (iv) ………………………………………………………………………………….

   (v) …………………………………………………………………………………….

   Je aliwahi kutibiwa? NDIYO ☐ HAPANA ☐

   (a) Wapi (taja hospitali)…………………………………………………

   (b) Hakuwahi

   (c) Kama ndiyo toa maelezo mafupi kuhusu tatizo hilo.

   ......................................................................................................................................

   ......................................................................................................................................

   ......................................................................................................................................

   .....................................................................................................................................

| | |
|---|---|
| Sahihi………………………………… | Sahihi………………………………………… |
| Jina ………………………………………….. | Jina.……………………………………………….. |
| **Mzazi/mlezi** | **Mwanafunzi** |

## MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA M

## JINAI.

Mimi……………………………………………..(mwanafunzi),naahidi kuwa

sitajihusisha/sitashiriki katika kupanga,kufanya wala kushabikia migomo,fujo au ghasia zozot se

Sahihi…………………………………………..tarehe…………………………………

### SHULE YA SEKONDARI CHIUNGUTWA S.1338 CENTRE No. S.1338

### FOMU YA MZAZI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI NA MAELEKEZO YA MWANAO KUSOMA CHIUNGUTWA SEKONDARI

Mimi…………………………………….mzazi/mle wa …………………………………………nimesoma na kuelewa maelekezo yaliyopo kwenye fomu ya kujiunga na shule ya sekondari chidya. Hivyo ninakubaliana/sikubaliani mwanangu ajiuunge na asome chidya sekondari.

Sahihi…………………………………………   tarehe………………………………………

Jina la mkuu wa shule………………………………………   sahihi………………………………….

**KUMBUKUMBU MUHIMU ZA MWANAFUNZI**

**(IJAZWE KABLA YA KURIPOTI SHULENI)**

1. JINA LA MWANAFUNZI……………………………………………..

   Dini…………………………………Dhehebu………………………………

2. (a)Jina la baba/mlezi ………………………………Passportsize

   (b)Kazi ya baba/mlezi ……………………………….

   (c)Mahali anakoishi.

   Kijiji/Mtaa……………………………..Kata…………………

   Wilaya/Mji……………………………Mkoa…………………

   Namba ya simu…………………….Email……………………WhatsApp…………………….

3. (a)Jina la mama/mlezi………………………………Passportsize.

   (b)Kazi ya mama,mlezi…………………………………………… .......

   (c)Mahali anakoishi.

   Kijiji/Mtaa……………………………..Kata…………………

   Wilaya/Mji……………………………Mkoa…………………

   Namba ya simu…………………….Email……………………WhatsAp…………………

**B. NDUGU WA KARIBU**

| **NA.** | **JINA** | **UHUSIANO** | **MAHALI ANAPOISHI** | **SIMU NAMBA** |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |

NB: Njoo na picha za ndugu wote wa karibu

## VIFAA VIFUATAVYO VINAPATIKANA KWENYE DUKA KARIBU NA SHULE KAMA UTAPENDA

| VIFAA | BEI |
|---|---|
| 1. NET | 8000/= |
| 2. SHUKA YA BLUU AU PINK | 8000/= |
| 3. TRACK SUTI YA BLUE BAHARI | 25000/= |
| 4. RIM | 13000/= |
| 5. SOKSI | 1000 (KWA MOJA) |
| 6. SKETI YA SHULE | 28000/= |
| 7. GAUNI | 28000/= |
| 8. SURUALI | 25000/= |
| 9. T-SHIRT YA KUSHINDIA YENYE NEMBO | 10000/= |
| 10. T- SHIRT YA DARASANI | 15000/= |
| 11. JEMBE LENYE MPINI | 10000/= |
| 12. FAGIO NGUMU YA NJE YA MTI | 40000 KILA MOJA |
| 13. SABUNI LITA 5 | 8500/= |

## ORODHA YA VITABU VINAVYOTAKIWA KUNULIWA NA WAZAZI

- ❖ HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI
  - HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI KIDATO CHA TANO – TIE
- ❖ HISTORY
  - HISTORY ADVANCE STUDENTS BOOK FORM FIVE - TIE
  - HISTORY FOR HIGH SCHOOLS FORM FIVE – MADAYA
- ❖ ACADEMIC COMMUNICATION
  - ACADEMIC COMMUNICATION - MGONJA ME
  - ACADEMIC COMMUNICATION ADVANCE SECONDARY SCHOOL STUDENTS BOOK - TIE
- ❖ FASIHI YA KISWAHILI

- FASIHI YA KISWAHILI KIDATO CHA TANO – TIE

❖ ENGLISH LANGUAGE

- COMPETENCE AND LINGUISTICS – MGONJA M.E
- ADVANCE ENGLISH LANGUAGE - SHEDRACK NDAMBO

❖ LITERATURE IN ENGLISH

- LITERATURE IN ENGLISH BOOK FIVE AND SIX – TIE

❖ GEOGRAPHY

- GEOGRAPHY ADVANCE SECONDARY SCHOOL FORM FIVE - TIE